HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 13 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Machi, 2023

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

Miaka miwili ya Samia kicheko kwa wakulima



Mkulima Rizika Bolgias Ngonyani wa Mjini Madaba akitoka kununua mbolea ya ruzuku aina ya SA leo tarehe 21 Oktoba, 2022 kutoka kwa wakala Mtewele General Traders and Insurance Agent wa Mkoani Njombe anayesambaza mbolea katika mikoa ya Njombe na Songea

NDANI>>

TFRA yapata Mwenyekiti Mpya wa Bodi ya Wakurugenzi 5

Ruzuku ya mbolea yasaidia kuongeza tija kwenye kilimo – Mkuu wa Mkoa wa Mtwara 6

Mbolea ya ruzuku yapunguza gharama za uzalishaji zao la kahawa 9

Miaka miwili ya Rais Samia kicheko kwa wakulima, wamshukuru

"Kwa ya mbolea ya zuruku tulikuwa tunanunua mfuko wa Urea kwa shilingi 140,000/=, tulikuwa tunanunua mfuko mmoja wa mbolea ya CAN kwa shilingi 130,000/= kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na wasaidizi wake, Wizara ya Kilimo kwa juhudi kubwa waliyoifanya ya kutupa ruzuku ya mbolea.

Kabla ya ruzuku uendeshaji wa zao la nanasi ulikuwa juu sana kuliko faida lakini baada ya kupata ruzuku tumekuwa na nafuu na tunapata tija, mbolea ya ruzuku imetusaidia na kuturudisha kwenye nafasi nzuri kwani imepunguza yale makali yaliyokuwepo ya 140,000/=, 130,000/= na sasa tunanunua kwa shilingi elfu sabini (70,000/=) kwa mbolea ya DAP na Urea kwa shilingi elfu sitini (60,000). Serikali imefanya jambo kubwa sana.

Hayo ni maneno ya mkulima wa nanasi eneo la Kiwangwa na Mwenyekiti Msatafu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) tawi la Kiwangwa, Mkoani Pwani, Amiri Mkang'ata, akielezea furaha yake baada ya serikali kutoa ruzuku ya mbolea na hivyo kuwafanya wakulima kuweza kulima eneo kubwa tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita wa kilimo.

Naye Bwana shamba wa Kijiji cha Mwavi kata ya Fukayosi Wilayani Bagamoyo, Amiri Abdul Nyasa anasema, mpaka mwishoni mwa mwezi Februari, wakulima 733 wamesajiliwa na zoezi la usajili linaendelea kwa wakulima wanaolima mazao tofautitofauti. Anasema, Wakulima wa wilaya hiyo wanajihusisha Zaidi na kilimo cha nanasi linalowasaidia kununua chakula mara baada ya mauzo. Anaongeza kuw, baada ya wakulima kupata taarifa ya uwepo wa ruzuku ya mbolea wamejitokeza kwa wingi kushiriki kwenye shughuli za kilimo kwani wamekuwa na uhakika wa kumudu bei za mbolea.

Naye Mkulima wa kitunguu, mahindi, maharage na mbogamboga wa eneo la Mang'ola wilayani Karatu mkoani Manyara, Mustapha Mbwambo anasema amepata nafuu sana ya uzalishaji wa kitunguu baada ya serikali kuanza kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima katika msimu wa kilimo 2022/23.

Mbwambo anasema, walipoanza msimu mwezi Juni, 2022 gharama ya mbolea ilikuwa juu sana na ilipanda ghafla na hivyo kuwaathiri kwenye shughuli zao za uzalishaji kutokana na ekari moja ya kitunguu kuhitaji mifuko 12 ya mbolea ambapo gharama ilikuwa juu sana na kueleza kupewa ruzuku ya mbolea kumewapunguzia mzigo huo kwa zaidi ya nusu ya gharama ya uzalishaji na kuwawezesha kuongeza maeneo ya kilimo.

Rais, wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alizindua mpango wa Ruzuku ya mbolea mnamo tarehe 8 mwezi Agosti, 2022 wakati wa maadhimisho ya sikukuu ya wakulima yaliyofanyika katika viwanja vya Mwakangale Jijini Mbeya na kuwataka Wizara ya Kilimo kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuanza utekelezaji wa mpango huo mnamo tarehe 15 Agosti, 2022.

Sababu ya Serikali kuja na Mpango wa mbolea ya ruzuku

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo anasema, kufuatia kupanda kwa bei ya mbolea kwenye soko la dunia na kuwafanya wakulima wengi kutoweza kumudu gharama za mbolea, Serikali ya Awamu ya sita ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 150 ili kugharamia ruzuku kwa msimu wa kilimo wa 2022/2023.

Anasema, Mwaka wa fedha 2020/2021 na 2021/2022 gharama za mbolea zilipanda kwa ghafla na wakulima walinunua bidhaa hiyo kwa bei ya kuanzia shilingi 1010,000 hadi 150,000 kufuatana na umbali anaonunulia bidhaa hiyo na kubainisha kuwa kutolewa kwa ruzuku kumepelekea nafuu ya zaidi ya nusu ya bei waliyonunulia mbolea miaka ya nyuma.

Dkt. Ngailo anaeleza kuwa, utoaji wa ruzuku umezingatia mahitaji halisi ya mkulima wa Tanzania kulingana na taarifa

za usajili na Bajeti ya Serikali na kubainisha kuwa Mbolea zilizohusika katika Mpango wa serikali wa utoaji wa ruzuku ni zile za kupandia na kukuzia ikiwemo -- DAP na Urea. Anasema, mbolea hizo ni takribani asilimia 50 ya matumizi yote ya mbolea nchini. Mbolea za kupandia na kukuzia za aina nyingine zimehusishwa kwenye ruzuku kulingana na mahitaji ya soko. Katika kuhamasisha matumizi ya mbolea zinazozalishwa nchini, mbolea zetu zinazozalishwa na viwanda vya ndani zimeingizwa kwenye mpango wa ruzuku kutokana na mahitaji ya soko.

Katika kuhakikisha malengo ya kutoa ruzuku yanafikiwa, ikiwa ni pamoja na kuwanufaisha wakulima halisi, kuongeza ufanisi wa utoaji wa ruzuku, kupunguza mianya ya udanganyifu, rushwa, muda na gharama za usimamizi kutokana na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji wa mipango ya ruzuku kwa miaka iliyopita, serikali iliamua kutumia mfumo wa kidijitali kutekeleza mpango wa ruzuku ya mbolea kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Dkt. Ngailo anaeleza.

Anaendelea kueleza kuwa, mfumo umetumia programu maalum ya kidigitali, au kwa Kiingereza, Digital Platform, kuratibu shughuli zote za utekelezaji ruzuku kuanzia utambuzi wa washiriki wa mfumo wakiwemo waingizaji na wazalishaji wa mbolea, wafanyabiashara, wakulima na aina za mbolea zitakazokuwa katika mpango wa ruzuku; kuratibu usambazaji; uuzaji wa mbolea kwa wakulima; na malipo ya ruzuku ya mbolea.

Dkt. Ngailo anabainisha kuwa, hadi kufikia mweziMachi, 2023 waingizaji wa mbolea 28 wamesajiliwa, wazalishaji 3, mawakala na wasambazaji wa mbolea 3,303 watakaotumika kusambaza mbolea katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara wamesajiliwa.

Aidha, anaeleza kuwa, mpaka kufikia mweziMachi, 2023 Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa imesajili jumla

Miaka miwili ya Rais Samia kicheko kwa wakulima, wamshukuru

ya wakulima 3,264,440 ambao wana vigezo vyote vya kunufaika na mbolea za ruzuku.

Kuongezeka kwa viwanda vya kutengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (fertilizer suppliments)

Akizungumzia kuhusu ongezeko la viwanda vya mbolea navisaidizi vyake, Dkt. Ngailo anaeleza kuwa, kutokana na utashi wa kisiasa na uhamasishaji uliofanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kumekuwa na jumla ya viwanda kumi na saba (17) vinavyozalisha aina mbalimbali za mbolea na visaidizi vyake. Kati ya viwanda 16 viwanda 3 huzalisha visaidizi vya mbolea (chokaa mazao na gypsum) vilivyoko mikoa ya Dodoma na Tanga viwanda 14 vinatengeneza mbolea za punje na maji ambapo kati ya hivyo 10 hutengeneza mbolea za maji na 6 hutengeneza mbolea za punje.

Aidha, Rais Dkt. Samia na serikali yake wameendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza ambapo mwekezaji kutoka nchini Burundi yupo katika hatua za mwisho za ujenzi wa kiwanda cha Itracom Fertilizer LTD kinachojengwa Nala Jijini Dodoma ambacho tayari kimeanza uzalishaji wa tani 200,000 kwa mwaka na baada ya mitambo yote, kiwanda kitazalisha tani 1,000,000 za mbolea na tani 300,000 za chokaa na hivyo kusaidia kupunguza utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi.

Ujenzi wa maabara kupima mbolea (Specialized fertilizer laboratory)

Dkt. Ngailo anaeleza kuwa, Mamlaka imekuwa ikitumia maabara za taasisi nyingine kupima ubora wa mbolea ambapo kumekuwa na ucheleweshaji wa kutoa majibu na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya udhibiti.

Anasema, ndani ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mamlaka ilitengewa bajeti na kuanza kutekeleza ujenzi wa maabara ya mbolea kwa njia ya force account ambapo hadi mwezi Februari 2023 ujenzi wake umefikia asilimia 95.

Anaongeza kuwa, uwepo wa Maabara ya mbolea utaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka na inatarajiwa kutumiwa na nchi jirani za Malawi, Zambia, DrC, Burundi na Rwanda na hivyo

Muonekano wa maabara ya mbolea inayojengwa kwa mfumo wa force account baada ya Serikali kutenga kiasi cha shilingi milioni 968,582,213 ili kutekeleza mradi huo utakaonufaisha taifa na nchi Jirani za Jamhuri ya demokrasia ya Kongo, Malawi, Burundi, Uganda na Rwanda.

Miaka miwili ya Rais Samia kicheko kwa wakulima, wamshukuru

kuongeza mapato ya nchi.

Hali ya upatikanaji wa mbolea

Akielezea kuhusu hali ya upatikanaji wa mbolea nchini ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Dkt. Samia, Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Ndani na Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja, Joseph Charos anasema kwa mwaka 2020/2021 hali ya upatikanaji wa mbolea ilikuwa ni tani 546,818 ambapo matumizi yalikuwa tani 475,870 na mpaka kufikia Januari, 2023 hali ya upatikanaji wa mbolea nchini imeanda na kufikia tani 678,528 sawa na asilimia 102 ya mahitaji ya mbolea ndani ya nchi ambapo matumizi yanakadiriwa kuwa tani 667,730 ifikapo mwezi June 2023 tunapomaliza msimu wa kilimo kwa mwaka 20222/2023.

Hali ya Udhibiti wa Mbolea nchini

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti, Happines Mbele anasema, mifumo ya udhibiti wa mbolea Nchini imeendelea kuimarishwa na kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mbolea bora kwa bei nafuu na kwa wakati. ndani ya miaka miwili ya Rais, Dkt. Samia. Anasema, Udhibiti umewezekana kufuatia kuongezeka kwa idadi ya wakaguzi wa mbolea nchini, kusajili wafanyabiashara wa mbolea na kutoa Mafunzo ya mara kwa mara juu ya mfumo wa uendeshaji wa biashara ya mbolea.

Anaongeza kuwa, kuanzia mwaka 2012 mpaka sasa kuna wakaguzi wa mbolea 140 kutoka katika Ofisi za Mamlaka na Halmashauri za Wilaya, Aidha, Maafisa kilimo 59 kati ya 140 walipata mafunzo ya ukaguzi na wanasubiri kutangazwa kwenye gazeti la serikali ili waendelee na uendelea na jukumu la Kudhibiti ubora wa mbolea.

Kuongezeka kwa idadi ya wafanyabiashara wa mbolea

Mafanikio mengine ndani ya tasnia ya mbolea chini ya uongozi wa Rais. Dkt. Samia ni kuongezeka kwa wafanyabiashara wa mbolea nchini. Bi. Mbele anaeleza kuwa, kufuatia uwepo wa mazingira rafiki ya biashara ndani ya nchi, idadi ya wafanyabiashara wa mbolea imeongezeka kutoka wafanyabiashara 1691 mwaka 2020/2021 hadi kufikia wafanyabiashara 4,776 mweziMachi, 2023. Anasema hayo ni mafanikio makubwa kwani yanaongeza nguvu ya usambazaji wa bidhaa hiyo kwa wakulima.

Kuongezeka kwa matumizi ya mbolea

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa matumizi ya mbolea ambapo yameongezeka kutoka tani 426,550.41 mwaka 2021/ 2022 hadi zaidi ya tani 667,730 kwa mwaka 2022/2023 ambapo bado msimu wa kilimo na mahitaji ya mbolea sokoni yanaendelea. Inaelezwa ongezeko hilo limetokana na utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya mbolea ulioamsha hari ya wakulima kuongeza maeneo yao ya kilimo na elimu a matumizi sahihi ya mbolea inayotolewa na Mamlaka kwa wakulima ili kuwawezesha kuongeza tija kwenye kilimo chao

Kufunguliwa kwa ofisi za kanda

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi, Victoria Elangwa anaeleza kuwa, miaka miwili iliopita Mamlaka ilikuwa na ofisi moja tu ambayo ndiyo ilikuwa makao makuu ya Mamlaka Jijini Dar esSalaam jambo ambalo lilikuwa likitumia muda mrefu kwa wadau kupata huduma ambazo zingewachukua muda mfupi kuzipata endapo wangekuwa na ofisi katika maeneo Jirani na wanakofanyia shughuli zao.

Anasema ndani ya miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mamlaka ilifanikiwa kufungua ofisi tano za Kanda ikiwa ni Kanda ya Nyanda za juu kusini (Mbeya), Kanda ya Mashariki (Dar Es Salaam) Kanda ya Kati (Tabora), Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza).

Kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma

Kwa upande wake, Meneja wa Kitengo cha Tehama, Robert Mtendamema anaeleza kuwa, ndani ya miaka miwili ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan Mamlaka imefanikiwa kuboresha mfumo wa utoaji wa huduma kwa wadau wake ambapo huduma zote zinatolewa kupitia Mfumo wa Kimtandao wa Mbolea- (FIS).

Anaeleza kuwa, mfumo huo unahudumia wadau ikiwa ni pamoja na wanaohitaji kujisajili kufanya biashara ya mbolea, kusajili mbolea mpya, waingizaji wapya wa mbolea na wale wanaowasilisha maombi ya vibali vya kutoa na kuingiza mbolea nchini ambapo awali huduma zote zilikuwa zikitolewa kwa mfumo wa analojia na hivyo kutumia muda mrefu na kuhusisha kusafiri ili kukamilisha mahitaji ya wadau.

Mafanikio haya yanapelekea Agenda 10/30: Kilimo ni Biashara ikibeba maana ya kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la taifa na kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 kuwa halisi kufuatia tija inayopatikana kupitia uimarishaji wa tasnia ya mbolea nchini.

TFRA yapata Mwenyekiti Mpya wa Bodi ya Wakurugenzi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amemteua Ndug. Anthony Dialo kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA)

Uteuzi huo uliotangazwa tarehe 14Machi, 2023 na Idara ya Mawasiliano Ikulu umeziba pengo lililokuwepo baada ya Mwenyekiti aliyepita Prof. Anthony Mshandete kumaliza muda wake.

Menejimenti na watumishi wote wa TFRA wanakupongeza na kukukaribisha wewe na wajumbe watakaoteuliwa na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe ili kujumuika katika shughuli ya kuwahudumia watanzania

Ruzuku ya mbolea yasaidia kuongeza tija kwenye kilimo – Mkuu wa Mkoa wa Mtwara

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza ofisini kwake Mkoani Mtwara wakati wa mahojiano maalum na wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) waliofika ofisini kwake kwa lengo la kutathmini namna mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku unavyotekelezwa mkoani humo tarehe 10Machi, 2023.

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas Ahmed alieleza kuwa, ruzuku ya mbolea inayotelewa na Serikali imesaidia kuongeza tija kwa wakulima ambapo idadi kubwa ya wakulima wamejitokeza na kuchangamkia fursa hiyo, hatua ambayo imechangia katika kumkwamua mkulima na kukuza pato la mkoa huo.

Kanali Abbas alitoa kauli hiyo ofisini kwake Mjini Mtwara katika mahojiano maalum na wataalamu kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) ikiwa ni aliyekuwa Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kusini, Dkt. Asheri Kalala aliyeambatana na Kaimu Meneja wa Kitengo cha Uhusiano, Mawasiliano na Elimu Bi. Matilda Kasanga na kueleza uamuzi wa Serikali wa kutoa ruzuku ya mbolea inapaswa kuungwa mkono na kila mtanzania kwani imempunguzia mkulima mzigo mkubwa wa gharama za uzalishaji.

Pia Mkuu wa Mkoa Kanali Abbas alieleza kuwa, kabla ya kuanza kutumia mfumo wa ruzuku mkulima alilazimika kununua kg. 50 za mbolea kwa gharamaya shilingi 140,000 lakini baada ya serikali kuanza kusambaza mbolea ya ruzuku, hivi sasa mkulima anapata kiwango kile kile cha mbolea kwa gharama ya shilingi 70,000 tu.

“Kwa dhati kabisa naishukuru serikali inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wakuinua sekta ya kilimo, ili iweze kutoa tafsiri halisi ya kuchangia kukuza uchumi na pato la taifa kwa ujumla” alisema Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

Halikadhalika, akizungumza kuhusu mchango wa sekta ya kilimo katika pato la Mkoa, Kanali Abbas alisema kati ya mwaka 2021/2022 pato la Mkoa lilikuwa shillingi trilioni 3.4 lakini kutokana na maboresho yaliyofanyika katika sekta ya kilimo hivi sasa pato

limepanda na kufikia shilingi trillion 4, ongezeko ambalo pia limechangiwa na uzalishaji wa mazao ya kimkakati ikiwemo korosho na ufuta.

"Sisi Mtwara tuna eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 17,620 ndani ya eneo hilo jumla ya hekta 1,672,000 ndizo zinafaa kwa kilimo, lakini sio zote zinazotumika kuzalisha" aliongeza Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

"Hivyo sisi tumejiwekea mikakati kama Mkoa itakayotusaidia kuongeza tija katika sekta hii, kwanza tunahakikisha tunahamasisha wakulima wetu kujisajili katika kanzi data, ambapo awali tulikadiria kusajili wakulima 77,901 lakini tumejikuta tunavuka lengo kwa kusajili wakulima 88,678. Pia tunahakikisha wataalamu wetu wa kilimo (Maafisa Ugani) wanawatembelea wakulima na kuwapa elimu" alisisitiza Kanali Ahmed Abbas Ahmed.

Kanali Abbas aliongeza kuwa, serikali ya Mkoa itawasiliana na TFRA ili kuona uwezekano wa kuvitumia vyama vya msingi vya ushirika ambayo ndio viko karibu zaidi na wakulima, ILI vishiriki katika zoezi la kugawa mbolea ya ruzuku ili kumpunguzia adha mkulima ambaye amekuwa

Aliyekuwa Kaimu Meneja wa TFRA kanda ya Kusini Dkt. Asheri Kalala akizungumza na wanahabari wakati wa ziara ya kikazi mikoa ya kusini iliyolenga kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mbolea za ruzuku kwa mikoa hiyo katikakti ya mwezi Februari.

Mkulima wa Kata ya Mnongodi Halmashauri ya Nanyamba Mkoani Mtwara, Mohamed Salum akitoka na mfuko wa mbolea mara baada ya kununua katika ghala la ETG mkoani Mtwara.

Afisa Mauzo wa Kampuni la Mbolea la ETG Input mkoani Mtwara akizungumza na wataalam wa Habari akitoa tathmini ya matumizi ya mbolea kwa wakulima wa mkoa wa Mtwara kwa mwaka 2022/2023 kwa wataalam wa Habari kutoka TFRA waliotembelea ghala hilo.

akilazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

"kwa vile nyinyi ndio wawakilishi wa Wizara naomba mpeleke ombi langu la kuongeza vituo vya kusambazia mbolea ya ruzuku, sisi Mkoa tutawahamasisha wadau wanaohitaji kuwa mawakala wajitokeze na kusaidia kusabaza mbolea kwa wakulima, tutaendelea na uhamasishaji wa matumizi sahihi ya mbolea na niiombe Mamlaka kupanua wigo wa kutoa elimu hiyo kwa wakulima" alisisitiza Kanali Ahmed Abbas.

Pia, Kanali Ahmed Abbas aliitumia fursa hiyo kuwahamasisha vijana kuchangamkia fursa ya kuingia katika sekta ya kilimo kama ambavyo serikali ya awamu ya sita imekuwa ikiwahamasisha na kuahidi kuwapatia ardhi na elimu ya kuendesha kilimo kwa tija.

Kwa upande wake, aliyekuwa Kaimu Meneja TFRA Kanda ya Kusini Dkt. Asheri Kalala alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa tayari Wizara ya kilimo imeandaa utaratibu mzuri utakaorahisisha upatikanaji wa mbolea katika maeneo yote nchini.

"Mhe Mkuu wa Mkoa kweli kabisa kuna baadhi ya maeneo wakulima wamekuwa wakisafiri umbali mrefu kufuata mbolea lakini baada ya Wizara kubaini changamoto hiyo, tayari imeviagiza vyama vya ushirika kuwatembelea wakulima na kupata mahitaji yao na kisha kuwasiliana na Mamlaka ili kusajiliwa na kupata kibali cha kuwahudumia hii itasaidia kupunguza adha ya msongamano katika vituo halikadhalika itawapunguzia kusafiri umbali mrefu" aliongeza Dkt. Kalala.

Kuhusu mkakati wa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya mbolea, Dkt. Kalala amesema kuwa wataalamu kutoka TFRA wameanza kutoa elimu hiyo katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo msimu wa kilimo wa Mwaka 2021/2022 walitoa elimu kupitia mashamba darasa hatua ambayo alikiri imechangia kuongeza kiwango cha uzalishaji na matumizi ya mbolea kwa wakulima wa mikoa ya Lindi na Mtwara.

Kwa upande wake, Afisa Mauzo wa Kampuni la Mbolea la ETG Input Mkoa wa Mtwara Bi. Neema Minja alisema kabla ya kutangazwa ruzuku ya mbolea walikuwa wakiuza chini ya tani 100 za mbolea lakini baada ya kutangazwa ruzuku ya mbolea mpaka mwishoni mwa mwezi Januari 2023 wamesambaza kiasi cha tani 300 za mbolea nab ado uhitaji wa mbolea ni mkubwa.

Mbolea ya ruzuku yapunguza gharama za uzalishaji zao la kahawa

Imeelezwa kuwa mpango wa mbolea ya ruzuku umeleta nafuu kubwa kwenye ahughuli za uzalishaji wa kahawa kwa kampuni ya kilimo cha kahawa ya Karatu Coffee Eatate LTD iliyoko Wilaya ya Karatu mkoani Arusha.

Kabla ya serikali kuja na mpango wa mbolea ya ruzuku kampuni ilikuwa ikitumia kiasi cha ahilingi milioni 250 hadi 300 kwa ajili ya mbolea lakini kwa masimu wa kilimo 2022/2023 kiasi cha shilingi milioni 120 hadi 140 kimetumika na kutoa nafuu kubwa kwenye uzalishaji.

Hayo yameelezwa na Meneja wa shamba hilo, Ladislaus Kauku alipofanya mahojiano na wanahabari kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania shamabni kwake, mahojiano yaliyolenga kujua manufaa aliyopata kutokana na uwepo wa mbolea za ruzuku.

Kauku alieleza kuwa, mpaka sasa wamenunua mifuko 1400 ya mbolea za ruzuku mifuko 700 mbolea ya Urea na mifuko mingine 700 ya mbolea aina ya NPK.

Alieleza kuwa wameshaweka mbolea ya majani tunasubiri awamu aina ya NPK kwa ajili ya majani wanasubiri mvua inyeshe ili waweke mbolea awamu ya pili kwa ajili ya mbegu.

"Mwaka huu tunatarajia kuzalisha vizuri kufuatia ukweli kuwa mbolea tunayo ya kutosha" Kauku alisema

"Uwepo wa mbolea ya ruzuku kutatuwezesha kuhudumia shamba vizuri na kuzalisha kahawa bora kutakakopelekea kuzalisha kahawa nzuri" Kauku aliongeza.

Akielezea upande wa mavuno, Kauku anasema mavuno kwa shamba zima ni tani 150 - 180 kwa msimu uliopita wa kilimo na kubainisha kuwa kwa mwaka huu wanatarajia kuvuna tani 200 hadi 250.

" Mbolea ya ruzuku inasaidia sana si kwa kahawa tu na hata kwa mazao mengine na hivyo kupunguza bei ya nafaka kufuatia wingi wa mazao"Kauku ameendelea kusisitiza manufaa ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Karia Magaro anasema mchango wa mazao kwenye mapato ya wilaya ni bilioni 2.4 na kueleza uwepo wa ruzuku ya mbolea utapelekea kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kilimo kwani wakulima wameongeza maeneo ya kilimo.

Katika msimu wa mwaka 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea inayoendelea kutolewa kwa wakulima wote nchini kwa lengo la kupunguza makali ya bei ya mbolea, kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani. Utoaji wa ruzuku umezingatia mahitaji halisi ya mkulima kulingana na taarifa za usajili zilizotolewa na wakulima. Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania Dkt. Staphan Ngailo anazungumza na **MWANDISHI WETU** kuhusu utekelezaji wa mpango huo ulioanza mwezi Agosti 2022.

Swali: **Hadi sasa ni wakulima wangapi wamesajiliwa kwenye mfumo huu wa kupokea ruzuku ya mbolea?**
Jibu: Wakulima walisajiliwa kwenye hadi sasa kwenye mfumo ni 2,920,853 na wakulima 710,021 wamenufaika na ruzuku ya mbolea mpaka kufikia Februari 23, 2023.

Swali : Je, ni hatua zipi za kisheria zimechukuliwa kwa wanaouza mbolea kinyume cha bei elekezi?
Jibu: Hatua zinazochukuliwa ni zile za kisheria zilizoainishwa na Sheria ya usimamizi wa mbolea na kanuni zake ikiwemo kufutiwa leseni na kwa wale wenye makosa yenye viashiria vya kijinai wanafikishwa katika vyombo vya dola kwa hatua zaidi za kisheria

Swali: Je, upangaji wa bei ya mbolea nishirikishi? Inawashirikisha wadau wote kama wazalishaji na wauzaji wa mbolea hiyo ya ruzuku?
Jibu: ndio upangaji wa bei zote za mbolea unashirikisha wadau wote wa mbalea, hii ni kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia manunuzi ya mbolea kwa Pamoja (Bulk Procurement System) inayotaka kushirikisha wadau wa mbolea katika upangaji wa bei elekezi kabla ya bei elekezi kutangazwa.

Swali: Wakulima wengi wa maeneo mbalimbali nchini, hasa katika mikoa ya nyanda za juu kusini ikiwemo Iringa Njombe na Mbeya wanalalamika kwa kutopata mbolea za ruzuku Kwa wakati na wengine kutokupata kabisa Kama mamlaka mnalizungumziaje hili?
Jibu: Kwa mujibu wa takwimu za kimfumo mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya nimiongoni mwa Mikoa inayoongoza kwa kunufaika na mbolea ya ruzuku. Kwa mfano katika mkoa wa Njombe wakulima waliosajiliwa ni 186,737 kati yao wakulima 118,995 wamenufaika na mbolea ya ruzuku ambayo ni sawa na asilimia 63.72% ya wakulima wote waliosajiliwa.
Mkoa wa Mbeya wakulima waliosajiliwa ni 276,320 kati yao wakulima 86,129 wamenufaika na mbolea ya ruzuku ambayo ni sawa na asilimia 31.17% ya wakulima wote waliosajiliwa.
Mkoa wa Iringa wakulima waliosajiliwa ni 165,660 kati yao wakulima 118,995 wamenufaika na mbolea ya ruzuku ambayo ni sawa na asilimia 63.72% ya wakulima wote waliosajiliwa.
Pia takwimu zinaonyesha manunuzi ya Mikoa hii ni makubwa kupita miaka ya nyuma, Hii inachangiwa na kushuka kwa bei ya mbolea hadi kufikia 50,000 hadi 70,000.

Swali: Mpango wa ruzuku ya mbolea umetekelezwa kwa kiasi gani hapa nchini na wakulima wangapi wamenufaika?
Jibu: Mpango wa ruzuku unatekelezwa katika mikoa yote 26 hapa nchini katika msimu wa 2022 -2023. hadi sasa kwenye mfumo ni 2,920,853 na wakulima 710,021 wamenufaika na ruzuku ya mbolea mpaka kufikia Februari 23, 2023.

Swali: Katika zoezi hili la ruzuku ya mbolea Kwa wakulima je kuna mikoa iliyopewa kipaombele? kama ipo ni ipi na kwanini? vipi kuhusu mikoa ya Kanda ya kati Singia na Dododma?
Jibu: Kama nilivyokutangulia kusema hapo awali mpango huu wa ruzuku unatekelezwa nchini Nzima na kwa wakulima wote katika mikoa yote 26.

Swali: Nani hasa anahusika na huu mfumo wa kidigitali unaotumika katika utekelezaji wa ruzuku ya mbolea?
Jibu: Mfumo wa kidigitali unaotumika katika utekelezaji wa ruzuku ya mbolea ni Mfumo wa Serikali unaosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa niaba ya wizara ya Kilimo. Mfumo huu umefadhiliwa na Benki ya CRDB

Swali : Moja ya majukumu ya TFRA ni Kuingia mikataba ya makubaliano na makampuni ya mbolea yaliyosajiliwa kwa ajili ya kuuza mbolea ya ruzuku kwa wakulima, kumekuwa na taarifa Kwa makampuni hayo kuweka mgomo wa chini chini wa kuuza mbolea kutokana na kuidai Serikali pesa kiasi Cha shilingi Bilioni 325, kama Mamlaka inayohisika na Kusajili haya makampuni je taarifa hizi ni za kweli? **na kama kweli kwa nini Serikali imehaija walipa.**
Jibu: Taarifa hizi hazina ukweli wowote, kwa sababu Makampuni yote yaliyoingia kwenye makubaliano kwa sasa yanaenedelea na usambazaji wa mbolea na kampuni hizi zimekwishaanza kulipwa madai yao na usambazaji wa mbolea kwa wakulima unaendela. Hadi kufikia leo tarehe 23 February jumla ya tani 290,200 zimeuzwa kwa wakulima nchini hadi kufikia Februari 23, 2023. Aidha, ni upotoshaji kuwa Serikali inadaiwa Shilingi Bilioni 325 kwani mpaka sasa hatujafikia kiasi hicho.

Mbolea ya ruzuku yapunguza gharama za uzalishaji zao la kahawa

Imeelezwa kuwa mpango wa mbolea ya ruzuku umeleta nafuu kubwa kwenye ahughuli za uzalishaji wa kahawa kwa kampuni ya kilimo cha kahawa ya Karatu Coffee Eatate LTD iliyoko Wilaya ya Karatu mkoani Arusha.

Kabla ya serikali kuja na mpango wa mbolea ya ruzuku kampuni ilikuwa ikitumia kiasi cha ahilingi milioni 250 hadi 300 kwa ajili ya mbolea lakini kwa masimu wa kilimo 2022/2023 kiasi cha shilingi milioni 120 hadi 140 kimetumika na kutoa nafuu kubwa kwenye uzalishaji.

Hayo yameelezwa na Meneja wa shamba hilo, Ladislaus Kauku alipofanya mahojiano na wanahabari kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania shamabni kwake, mahojiano yaliyolenga kujua manufaa aliyopata kutokana na uwepo wa mbolea za ruzuku.

Kauku alieleza kuwa, mpaka sasa wamenunua mifuko 1400 ya mbolea za ruzuku mifuko 700 mbolea ya Urea na mifuko mingine 700 ya mbolea aina ya NPK.

Alieleza kuwa wameshaweka mbolea ya majani tunasubiri awamu aina ya NPK kwa ajili ya majani wanasubiri mvua inyeshe ili waweke mbolea awamu ya pili kwa ajili ya mbegu.

"Mwaka huu tunatarajia kuzalisha vizuri kufuatia ukweli kuwa mbolea tunayo ya kutosha" Kauku alisema

"Uwepo wa mbolea ya ruzuku kutatuwezesha kuhudumia shamba vizuri na kuzalisha kahawa bora kutakakopelekea kuzalisha kahawa nzuri" Kauku aliongeza.

Akielezea upande wa mavuno, Kauku anasema mavuno kwa shamba zima ni tani 150 - 180 kwa msimu uliopita wa kilimo na kubainisha kuwa kwa mwaka huu wanatarajia kuvuna tani 200 hadi 250.

" Mbolea ya ruzuku inasaidia sana si kwa kahawa tu na hata kwa mazao mengine na hivyo kupunguza bei ya nafaka kufuatia wingi wa mazao"Kauku ameendelea kusisitiza manufaa ya mbolea ya ruzuku kwa wakulima.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, Karia Magaro anasema mchango wa mazao kwenye mapato ya wilaya ni bilioni 2.4 na kueleza uwepo wa ruzuku ya mbolea utapelekea kuongezeka kwa mapato yatokanayo na kilimo kwani wakulima wameongeza maeneo ya kilimo.

Mfumo Ruzuku ya mbolea waondoa biashara haramu

Imeelezwa kwamba, mfumo unaotumika kusambaza mbolea za ruzuku umesaidia kuondoa biashara haramu (black market) ya mbolea na kupunguza ushindani kwenye soko la ndani kufuatia bei ya bidhaa hiyo kwa wakulima kuwa ni moja nchi nzima.

Hayo yamebainishwa na Afisa Masoko wa kampuni la mbolea la Mohamed Enterprise Kanda ya Kaskazini, Richard Kika alipokuwa akizungumza na wanahabari waliofika lilipo ghala la mbolea ya kampuni hiyo Jijini Arusha.

"Mfumo umeondoa biashara ya magendo na tabia za watu kuhodhi mbolea ili baadaye wauze kwa bei ya juu" Kika alisisitiza.

Alisema, mfumo huo pia umewasaidia wafanyabiashara na serikali kwa ujumla kupata takwimu sahihi za kiasi cha mbolea kilichouzwa kwa wakulima na kiasi kilichopo kwa ajili ya usambazaji.

Aidha, Abbas alieleza kuwa, mfumo wa mbolea ya ruzuku umewasaidia wakulima kununua bidhaa hiyo kwa bei halali tofauti na awali ambapo kila mfanyabiashara aliuza bei yake ilimradi alizingatia bei elekezi iliyotolewa na serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, (TFRA).

Pamoja na hayo, Afisa Masoko Kika awali kampuni lao lilikuwa likijihusisha na biashara ya mbolea Jijini Dar es Salaam pekee lakini kuanza mfumo wa mbolea zaruzuku uanze wamefanikiwa kufungua matawi mengine katika mikoa

mbalimbali na kueleza tawi la Arusha lilifunguliwa Mwezi September, 2022.

Aliongeza kuwa, kiasi cha mbolea kilichouzwa mpaka mwishoni mwa mwezi Januari, 2023 ni tani 782 ambapo msimu wa kilimo mkoani humo bado haujaanza na kubakiwa na mifuko 623 ya mbolea ghalani huku wakitarajia kuongeza mauzo kutokana na mwitikio wa wakulima wa kutumia mbolea kwa msimu huu wa kilimo.

Aidha, Kika alieleza kuwa, shehena nyingine ya mbolea inaendelea kuletwa ili kukidhi mahitaji ya wakulima kwa msimu wa kilimo unaoanza mwezi Februari kwa mikoa ya Kaskazini.

Tani 9,361.48 za mbolea za ruzuku kuwanufaisha wakulima Kilimanjaro

Wakulima waishukuru serikali

Zaidi ya Shilingi bilioni 17 zimetolewa na serikali ili kugharamia ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa Kanda ya Kaskazini mwa Tanzania kuanzia mwezi Agosti 2022 hadi sasa na kuwanufaisha wakulima wa mazao ya kibiashara, chakula ikiwa ni pamoja na mazao ya mbogamboga na matunda.

Kiasi cha tani 9,361 zambolea zimewafikia wakulima na kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji na tijakayika kilimo, kuimarisha shughuli za kilimo, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza upatikanaji wa malighafi za viwanda vya ndani.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Kaskazini, Gothard Liampawe alipokuwa akizungumza na wanahabari waliopiga kambi katika kanda anayoisimamia kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa mpango wa ruzuku za mbolea unaotekelezwa na Seriikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa msimu wa kilimo 2022/2023.

Liampawe amesema ruzuku hiyo itawanufaisha wakulima 1,309,199 wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga pindi usajili utakapokamilika na kubainisha mkoa wa Kilimanjaro umeongoza kwa kusajili wakulima158,399 kwenye mfumo wa kidijitali baada ya daftari 2160 za kusajili wakulima kusambazwa kwenye vijiji vya mkoa huo na kufikia malengo kwa asilimia 39.

Ameeleza kuwa, ufanisi wa watendaji wa mkoa huo katika zoezi la kusajili wakulima kumeongeza hamasa kwa wafanyabiashara wa mbolea kupanua wigo wa biashara kwa kufungua vituo ambapo mpaka sasa wapo mawakala 35 waliosajiliwa kuuza mbolea mkoani humo.

Tani 9,361.48 za mbolea za ruzuku kuwanufaisha wakulima Kilimanjaro

Liampawe aliongeza kuwa mpaka kufikia tarehe 27 Januari, 2023 kiasi cha tani 7,477.75 za mbolea zilikuwa zimesambazwa kwa wakulima kwa mkoa wa Kilimanjaro huku wakitarajia kuuza kiasi cha tani 13,173.65 kufikia mwezi Juni 2023 mwisho wa msimu wa kilimo kwa mwaka 2022/2023.

Liampawe aliongeza kuwa, tangu kuanza kwa utekelezaji wa mpango wa ruzuku, mkoa wa Kilimanjaro umenufaika kwa mifuko 190,551 sawa na tani 9,361.48 za mbolea za ruzuku.

Kwa upande wao wakulima wa maeneo mbalimbali ya mkoa huo wakizungumza kwa nyakati tofauti waliishukuru serikali kwa kuja na mpango wa mbolea za ruzuku na kueleza umewapunguzia mzigo mzito wa kugharamia mbolea.

Akizungumza kwa niaba ya wanaushirika wa skimu ya Kaloleni, Mwenyekiti wa skimu na mkulima Mohamed Nditi alisema skimu yao ina ukubwa wa hekta 250 zilizogawanywa kwa wakulima 400 walionufaika na mbolea za ruzuku.

"Tunaomba zoezi la mbolea za ruzuku liwe endelevu kwani imesaidia kuongeza uzalishaji kutoka tani 1.2 za mchele hadi tani 1.9 kwa ekari baada ya kutumia mbolea" aliongeza Nditi

Naye mkulima Kandida Urio kutoka Kaloleni Moshi, ameeleza kuwa, amefanya shughuli za kilimo kwa muda mrefu lakini hakuweza kufanikiwa kutokana na matumizi hafifu ya mbolea.

Kandida anasema ruzuku ya mbolea imeboresha kilimo chao na kueleza kuwa wamefanikiwa sana kwa kupata mbolea hizo za ruzuku.

Naye mkulima kijana, Suleiman Kushima anatoa shukrani zake kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha kupata mbolea za ruzuku na kueleza awali alikuwa akivuna gunia 17 kwa ekari lakini kwa sasa anavuna gunia 21 za mpunga.

"Mbolea ya ruzuku ilivyoletwa imetukomboa wengi kwa asilimia 99, tumeipokea vizuri na tumeitumia vizuri na kuongeza kipato na ninaamini kipato kitaongezeka zaidi" alisema mkulima Abdallah Kahumba.

TFRA IMEDHIBITI UINGIZWAJI HOLELA WA MBOLEA NCHINI

Na Pascal Dotto - MAELEZO

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Nchini (TFRA imeimarisha udhibiti wa mbolea kwa kuzuia mbolea zote ambazo zinaingizwa kwa njia ya magendo na kuruhusu wakulima kutumia mbolea zilizothibitishwa na Serikali kupitia mamlaka hiyo.

Akizungumza Jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Stephan Ngailo alisema kuwa mpaka sasa Serikali imefanikiwa kudhibiti uingizwaji wa mbolea ambayo haikidhi matumizi kwa ajili ya kilimo

“Sisi kama TFRA tutahakikisha kwamba hakuna matumizi ya mbolea isiyo na kiwango kwa wakulima nchini, kwa kuzingatia hilo TFRA imesajili mbolea 481 kufikiaMachi, 2023, wafanyabiashara wa mbolea wameongezeka kutoka 51 mwaka 2012/13 hadi kufikia wafanyabiashara 4,183, Februari 2023 hii imejenga uaminifu mkubwa kwa wakulima na kutumia mbolea katika uzalishaji wa mazao yao”, alisema Dkt. Ngailo.

Alisema kuwa kuimarishwa kwa usimamizi imewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka Tani 210,876

mwaka 2012 hadi kufikia tani 475,870 mwaka 2020/2021 na mpaka sasa TFRA inatumia mfumo wa utoaji huduma za mbolea (Fertilizer Information System-FIS), ili kurahisisha upatikanaji wa mbolea kwa wakulima nchini.

Aidha kutokana na uhamasishaji uliofanywa na unaoendelea kufanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mpaka sasa Tasnia ya Mbolea ina Viwanda 17 na kuwezesha uwekezaji kuwa mkubwa katika tasnia hiyo ambayo ni muhimu kwa wakulima nchini.

TFRA IMEDHIBITI UINGIZWAJI HOLELA WA MBOLEA NCHINI

"Mpaka sasa wawekezaji mbalimbali wamejitokeza akiwemo mwekezaji kutoka Burundi ambaye anajenga kiwanda kikubwa pale Dodoma, kampuni ya Petrochemical ya Ujerumani inayojenga kiwanda cha mbolea ya UREA kwa kutumia gesi asilia Mkoani Mtwara, hii itaongeza uzalishaji wa mbolea nchini na kuwezesha bei kuwa nzuri zaidi kwa wakulima wetu", Dkt. Ngailo.

Aliongeza kuwa ili kudhibiti kuwepo kwa mbolea ambayo haifai kwa matumizi TFRA ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa ujenzi wa maabara mahsusi ya kupima ubora wa mbolea zote zinazotengenezwa, kuingizwa na kutumika hapa nchini na mpaka Februari 2023, ujenzi wake umefikia asilimia 95.

Mwonekano wa maabara ya mbolea ikiwa ni aslimia 95 za kukamilika kwa ujenzi wake.

YALIYOJILI WAKATI WA MKUTANO WA WAANDISHI WA HABARI NA MKURUGENZI MTENDAJI, TFRA, DKT. STEPHAN NGAILO FABRUARI 23, 2023

#TFRA imeimarisha udhibiti wa mbolea nchini kwa kuzuia mbolea zote ambazo zinaingizwa kwa njia ya magendo na kuruhusu wakulima kutumia mbolea sahihi.

#Sisi kama TFRA tutahakikisha kwamba hakuna matumizi ya mbolea isiyo na kiwango kwa wakulima nchini.

#TFRA imesajili mbolea 481 kufikiaMachi, 2023 lakini pia wafanyabiashara wa mbolea wameongezeka kutoka 51 mwaka 2012/13 hadi kufikia wafanyabiashara 4,183 hadi kufikia Februari 2023.

#Baada ya TFRA kuimarisha usimamizi imewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka Tani 210,876 mwaka 2012 hadi kufikia tani 475,870 mwaka 2020/2021.

#TFRA imeimarisha mfumo wa utoaji huduma za mbolea ambapo kwa sasa mbolea zote zinatolewa kwa kutumia mfumo wa kimtandao (Fertilizer Information System-FIS).

Kutokana na uhamasishaji uliofanywa na unaoendelea kufanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mpaka sasa Tasnia ya Mbolea ina Viwanda 17 na kuwezesha matumizi ya mbole kuwa makubwa.

#Mpaka sasa wawekezaji mbalimbali wamejitokeza akiwemo mwekezaji kutoka Burundi ambaye anajenga kiwanda kikubwa pale Dodoma, kampuni ya Petrochemical ya Ujerumani inayojenga kiwanda cha mbolea ya UREA kwa kutumia gesi asilia Mkoani Mtwara.

#TFRA ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa ujenzi wa maabara mahsusi ya kupima ubora wa mbolea zote zinazotengenezwa, kuingizwa na kutumika hapa nchini na mpaka Februari 2023, ujenzi wake umefikia asilimia 95.

#Serikali ilipanga na kutenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kugharamia ruzuku ya mbolea katika msimu wa kilimo 2022/2023 iliyotolewa kwa wakulima wote nchini.

#Hadi kufikia mwezi Februari 2023, TFRA imesajili waingizaji wa mbolea 28, wazalishaji 3 ambao wanashiriki kuingiza, kuzalisha na kusambaza mbolea ya ruzuku msimu wa 2022/2023.

#TFRA pia imesajili mawakala 3,428 wanaosambaza na kuuza mbolea ya ruzuku katika mikoa 26 nchini na kufikia Februari 2023, wakulima 2, 916, 703 wamesajiliwa kwenye mfumo wa kupata namba maalum ya kununulia mbolea ya ruzuku.

TFRA inajivunia ongezeko la matumizi ya mbolea ambapo nyanda za juu kusini imeongoza kwa usajili wakulima 1,209,692, kanda ya kati 501,941, kanda ya ziwa 488,845 kanda ya kaskazini 423,921 na kanda ya mashariki 289,218.

#Bei ya mbolea zilizoko katika mfumo wa Ruzuku ni shilingi 50,000 hadi 70,000 kwa mbolea inayoingizwa kutoka nje ya nchi na shilingi 60,000 hadi 70,000 kwa mbolea inayozalishwa ndani ya nchi.

Hadi Februari 2023 jumla ya tani 290,200.525 zimeuzwa kwa jumla ya wakulima 710,021, pia tani 54,061 zimeuzwa nje ya mfumo wa mbolea ya ruzuku.

Imeandaliwa na Idara ya Habari-MAELEZO NA KITENGO CHA PRCE TFRA

Tanzania, Saudi Arabia waanza ushirikiano tasnia ya mbolea

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo ameshuhudia makabidhiano ya kontena lenye shehena ya mbolea kiasi cha tani 20 baina ya Mkurugenzi wa Kampuni la Mbolea la Taifa (TFC) Bw. Samwel Mshote na Mwenekiti na Meneja Mkuu wa kiwanda cha Surphur (Sulphur Factory-SAF) cha nchini Saudi Arabia Sheikh Nasser Bin Al Sahli.

Imeelezwa kuwa ujio wa kontena hilo ni matokeo ya mwaliko wa kutembelea kiwanda hicho uliotolewa kwa nchi ambapo nchi iliwakilishwa na Bi. Kanjel Mloba kutoka TFC na Bi. Happiness Mbelle kutoka TFRA na kuwawezesha kujifunza namna kiwanda hicho kinavyozalisha bidhaa za kilimo ikiwemo sulphur.

Akizungumza wakati wa hafla ya makabidhiano hayo, Mkurugenzi Mtendaji Dkt. Ngailo alisema shehena hiyo

Tanzania, Saudi Arabia waanza ushirikiano tasnia ya mbolea

imeletwa kwa ajili ya majaribio na kuidhibitisha mbolea hiyo endapo itakidhi viwango vya ubora unaofaa kwa matumizi ya kilimo na viwanda kwa wakulima na wawekezaji nchini.

Makabidhiano hayo yamefanyika katika ofisi za GSM Jijini Dar es Salaam ambako kontena lilihifadhiwa na wakala aliyehusika kupakua mzigo huo bandarini huku akiendelea na taratibu za kulitoa tayari kwa ajili ya majaribio kwa wakulima nchini.

Naye Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Samwel Mshote alisema kufuatia kampuni anayoisimamia kukasimiwa jukumu la uagizaji, usambazaji na uuzaji wa mbolea nchini mashirikiano hayo yamepanua wigo na kuwezesha kuwa na mahusiano ya kimkakati wa kuiwezesha wizara ya kilimo kuwa na wadau watakaochangia katika kukuza Sekta ya Kilimo.

Akizungumza kuhusu ziara waliyoifanya nchini Saudi Arabia Mwezi Novemba, 2022 Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa TFRA, Bi. Happiness Mbele alisema ziara hiyo imezaa matunda na kufungua wigo wa uwekezaji katika tasnia ya kilimo ikiwa ni Pamoja na ujenzi wa kiwanda cha mbolea Pamoja na uingizaji wa mbolea na viuatilifu.

Aidha, Bi Happiness alisema ziara hiyo imeimarisha mahusiano na kusaidia katika kuhakikisha Maabara ya mbolea ambayo ipo katika hatua za mwisho za ujenzi inakamilika na kufanya kazi iliyokusudiwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawaala TFC Bi. Kanjel Mloba, alieleza faida zilizotokana na ziara yao kuwa imezaa matunda ikiwa ni Pamoja na kuchochea ujenzi wa kiwanda cha viuatilifu (sulphur) na mbolea, imeongeza wigo wa kibiashara na kuhakikisha viuatilifu na mbolea bora zinawafikia wakulima na kupelekea uzalishaji wenye tija na hivyo kuongeza usalama wa chakula.